

Title	Miundo ya Sentensi zenye Kitenzi ‘-wa’ katika Kichaani : Kwa Kulinganisha na Kiswahili SanifuAK
Author(s)	Takemura, Keiko
Citation	スワヒリ&アフリカ研究. 27 P.53-P.63
Issue Date	2016
Text Version	publisher
URL	<a href="https://doi.org/10.18910/71116">https://doi.org/10.18910/71116</a>
DOI	10.18910/71116
rights	
Note	

***Osaka University Knowledge Archive : OUKA***

<https://ir.library.osaka-u.ac.jp/repo/ouka/all/>

# Miundo ya Sentensi zenye Kitenzi ‘-wa’ katika Kichaani<sup>1)</sup>

- Kwa Kulinganisha na Kiswahili Sanifu -

TAKEMURA Keiko

## 0. Utangulizi

Kama tulivyoona katika makala ya “Miundo ya Dhamira Matilaba na Dhamira Amri katika Kichaani” (Takemura 2015), Kiswahili kina lahaja nyingi kiasi na baadhi ya lahaja hizo tayari zimeshafanyiwa tafiti nyingi. Lakini bila ya shaka bado kuna mambo yasiyojulikana na kufafanuliwa, hata idadi ya lahaja inayotajwa katika makala zilizoandikwa (Stigand 1915, Bryan 1959, Mkude 1983, Nurse & Hinnebusch 1993), yaani lahaja 24, pia inasemekana kuwa haijahakikishwa bado.

Mimi mwenyewe nimefanya utafiti wa lahaja kadhaa za Kiswahili kwa muda wa zaidi ya miaka 10 katika Mkoa wa Kaskazini, kisiwani Unguja. Kijiji muhimu sana kwa utafiti wangu ni kijiji kinachoitwa Chaani. Kijiji hicho kiko katika Wilaya ya Kaskazini A, Mkoa wa Kaskazini, Unguja, yaani Kaskazini-Mashariki ya Mji Mkongwe, umbali wake ni kilomita 40 hivi kutoka mjini. Kijiji hicho na vijiji vingine vilivyoko karibu na Chaani inasemekana kuwa viliundwa na watu wanaotoka kisiwa cha Tumbatu. Wengi wa wanaoishi katika vijiji hivyo wametanabahi kwamba kuna tofauti baina ya Kiswahili wanachosema na Kiunguja-Mjini na wanadai kuwa Kiswahili chao kinafanana na Kitumbatu. Kwa kweli, kutokana na matokeo ya utafiti wangu<sup>2)</sup>, imehakikishwa kuwa lahaja za Kichaani na Kiunguja-Mjini zinatofautiana hata kisarufi na kimsamiati, na lahaja za Kichaani na Kitumbatu zinafanana.

Katika makala hii tutaangalia miundo ya sentensi za Kichaani zinazotumia kitenzi -wa ili kufafanua tofauti kubwa baina ya Kichaani na Kiswahili Sanifu. Kwanza tutazungumzia viambishi kadhaa vinavyotumiwa katika sentensi na muundo wa dhamira dhahiri katika Kichaani. Na tunapoandika Kichaani, tunafuata kanuni ya kuandika Kiswahili Sanifu. Ili kuhakikisha tofauti baina ya Kichaani na Kiswahili Sanifu, tutaonyesha mifano ya sentensi za Kichaani pamoja na tafsiri zake kwa Kiswahili Sanifu. Mifano yenye herufi ‘a’ ni sentensi za Kichaani, na yenye herufi ‘b’ ni sentensi za Kiswahili Sanifu. Na tafsiri za sentensi hizo kwa Kiingereza zinaambatanishwa juu.

---

<sup>1)</sup> Makala hii, msingi wake ni uwasilishaji wa Kiingereza niliufanya katika Warsha ya Kimataifa ya Lugha za Kibantu, mnamo tarehe 11/11/2012, mjini Osaka.

<sup>2)</sup> Nilifanya utafiti wangu huko kijijini Chaani mwezi wa 8 mwaka 2011, mwezi wa 8 mwaka 2012 na mwezi wa 8 mwaka 2013. Nitaandika makala nyingine juu ya matokeo ya utafiti huo.

## 1. Muundo wa Dhamira Dhahiri

Katika Kichaani, muundo wa dhamira dhahiri ni hivi:

kiambishi-kiima – kiambishi-njeo – kiambishi-yambwa – mzizi wa kitenzi – kiambishi-nyambulishi – kiishio

(1) ‘You write a letter to me.’

a. Ku-na-ni-andik-i-ya baruwa.

SM2SG-PRS-OM1SG-write-APPL-BF letter9

b. U-na-ni-andik-i-a barua.

SM2SG-PRS-OM1SG-write-APPL-BF letter9

Katika muundo huu, kiambishi-kiima, kiambishi-njeo, mzizi wa kitenzi na kiishio ndizo mofimu za msingi zisizokosekana. Kiambishi-kiima kinatokea kupatana na kiima cha sentensi na kiambishi-yambwa kinatokea kupatana na yambwa ya sentensi, lakini baadhi ya sentensi hazina kiima cheneyewe wala yambwa yenyewe, basi katika sentensi kama hizo kiambishi-kiima na kiambishi-yambwa kinafanya kazi ya kiwakilishi. Hasa ikiwa kiambishi-kiima ama kiambishi-yambwa ni kiambishi-nafsi, katika sentensi kiwakilishi-nafsi hakitokei kwa kawaida, na kikitokea kinafanya kazi ya kusisitiza.

Ikiwa nomino ya kiima ama ya yambwa ina maana ya ‘kiumbe’, hata kama nomino hii si ya ngeli ya 1 (umoja) au ya 2 (wingi), kiambishi-kiima ama kiambishi-yambwa sharti kiwe cha ngeli ya 1 au ya 2. Ikiwa sentensi yenyewe ni ya kukanusha, kiambishi-kiima lazima kiwe cha kukanusha.

<Jedwali la 1: Viambishi-njeo na Viishio vya Kichaani>

kiambishi-njeo		kiishio	
-na-	wakati uliopo	-a	msingi
-ta-	wakati ujao	-V	ukanushi wa wakati uliopo wakati uliopita
-∅-	wakati uliopita	-e	dhamira matilaba
-e-	ukanushi wa wakati uliopita		
-ma-	hali timilifu		
-sha-	hali timilifu kabisa		
-ja-	ukanushi wa hali timilifu		
-ka-	hali ya kufuatana, sharti, uambatani / kwa wakati mmoja		
-hu-	hali ya mazoea		
-nge-	hali ya sharti lisilotimia		
-ngali-	hali ya kuendelea		

Kinachoonyesha njeo ni kiambishi-njeo, lakini kwa baadhi ya njeo hata kiishio kinabadilika. Kwa mfano sentensi ya njeo iliyopita ina kiishio ambacho ni vokali sawa na vokali ya mwisho kabisa ya mzizi wa kitenzi. Hapo juu tunaonyesha njeo zote za Kichaani katika jedwali la 1. Kwa kawaida kiishio ni vokali moja, lakini ili kuepusha mfululizo wa vokali kadhaa, ikiwa sauti ya mwisho ya mzizi wa kitenzi ni vokali ama sauti ya mwisho ya kiambishi-nyambulishi ni vokali, /y/ inaingizwa kabla ya kiishio. Katika jedwali la juu ‘-V’ maana yake ni vokali sawa na vokali ya mwisho kabisa ya mzizi wa kitenzi.

(2) ‘I read a letter.’

a. Ni-som-o            baruwa.

SM1SG-read-PstF   letter9

b. Ni-li-som-a           baruwa.

SM1SG-PST-read-BF   letter9

Katika sentensi ya wakati uliopita kiishio chake ni vokali sawa na vokali ya mwisho kabisa ya mzizi wa kitenzi<sup>3)</sup>, lakini kama tulivyotaja hapo juu, ili kuepusha mfululizo wa vokali kadhaa, ikiwa sauti ya mwisho wa mzizi wa kitenzi ni vokali, /y/ inaingizwa kabla ya kiishio kama katika mfano (3).

(3) ‘She/he bought a book.’

a. Ka-nunu-yu        buku.

SM3SG-buy-PstF    book5

b. A-li-nunu-a        kitabu.

SM3SG-PST-buy-BF   book7

Lakini ikiwa sauti ya mwisho kabisa ya mzizi wa kitenzi ni vokali ‘e’ au ‘i’, /l/ inaingizwa kabla ya kiishio kama katika mfano (4) na (5).

(4) ‘We brought up Mwajuma.’

a. Tu-m-le-le            Mwajuma.

SM1PL-OM3SG-bring up-PstF   Mwajuma

b. Tu-li-m-le-a            Mwajuma.

SM1PL-PST-OM3SG-bring up-BF   Mwajuma

(5) ‘You (pl.) cried.’

a. Mu-li-li.

SM2PL-cry-PstF

---

<sup>3)</sup> Whiteley (1959) ametaja kuwa hata katika Kimtang’ata muundo wa sentensi ya wakati uliopita ni sawasawa na huu. Kimtang’ata kinasemwa si visiwani bali barani, kwa hivyo inasemekana kwamba unahitajika utafiti wa dhati wa lahaja nyingine nyingi za sehemu za bara hasa mkabala na kisiwa cha Unguja.

b. M-li-li-a.

SM2PL-PST-cry-BF

## 2. Muundo wa Sentensi zenye Kitenzi '-wa'

Sasa tuangalie sentensi zenye kitenzi '-wa' katika njeo mbalimbali kama wakati uliopo, wakati ujao, wakati uliopita, hali timilifu na hali timilifu kabisa.

### 2.1 Wakati Uliopo

(6) 'I'm at school.'

a. Ni-w-a-po                      skuli.  
SM1SG-be-BF-LOC16              school9

b. Ni-po                              shule-ni.  
SM1SG-LOC16                      school9-LOC

(7) 'He is in the house.'

a. Ka-w-a-mo                      nyumba-ni.  
SM3SG-be-BF-LOC18              house9-LOC

b. Yu-mo                              nyumba-ni.  
SM3SG-LOC18                      house9-LOC

Kama tunavyoona muundo ulioonyeshwa juu, katika Kichaani kwa 'Kauli ya Kuwa Pahala Fulani' lazima tutumie kitenzi -wa ingawa katika Kiswahili Sanifu hatutumii. Lakini katika kauli ya kukanusha hata Kichaani hakihitaji kitenzi -wa kama katika mifano (8) na (9).

(8) 'Table is not here.'

a. Meza hai-po                      pano.  
table9      NegSM9-LOC16              DEMN16

b. Meza hai-po                      hapa.  
table9      NegSM9-LOC16              DEMN16

(9) 'She/He is not at home.'

a. Ha-po                              nyumba-ni.  
NegSM3SG-LOC16              house9-LOC

b. Hayu-po                              nyumba-ni.  
NegSM3SG-LOC16              house9-LOC

### 2.2 Wakati Ujao

Tukiangalia mifano (10) na (11) inafahamika kwamba katika njeo ijayo hata Kichaani kinahitaji kiambishi -ku- kabla ya kitenzi -wa. Na kutokana na mfano (10) tunafahamu kuwa kabla

ya kiambishi cha wakati ujao kiambishi-kiima cha nafsi ya kwanza hakiwekwi. Katika kauli ya kukanusha hakuna tofauti kubwa baina ya Kichaani na Kiswahili Sanifu kama tunavyoona katika mifano (12) na (13).

- (10) 'Next year I will have a cow.'
- a. Mwaka-ni ta-ku-w-a na ng'ombe.  
year3-LOC FUT-INF-be-BF with cow9
- b. Mwaka-ni ni-ta-ku-w-a na ng'ombe.  
year3-LOC SM1SG-FUT-INF-be-BF with cow9
- (11) 'Tomorrow she/he will be a student.'
- a. Kesho ka-ta-ku-w-a mwanafuzi.  
tomorrow9 SM3SG-FUT-INF-be-BF student1
- b. Kesho a-ta-ku-w-a mwanafunzi.  
tomorrow9 SM3SG-FUT-INF-be-BF student1
- (12) 'Next year I will not have a cow.'
- a. Mwaka-ni si-ta-ku-w-a na ng'ombe.  
year3-LOC NegSM1SG-FUT-INF-be-BF with cow9
- b. Mwaka-ni si-ta-ku-w-a na ng'ombe.  
year3-LOC NegSM1SG-FUT-INF-be-BF with cow9
- (13) 'Tomorrow she/he will not be a student.'
- a. Kesho ha-ta-ku-w-a mwanafuzi.  
tomorrow9 NegSM3SG-FUT-INF-be-BF student1
- b. Kesho ha-ta-ku-w-a mwanafunzi.  
tomorrow9 NegSM3SG-FUT-INF-be-BF student1

### 2.3 Wakati Uliopita

- (14) 'Twenty years ago I had a cow.'
- a. Miyaka ishirini i-yo-pit-a nyevu (< ni-evu) na ng'ombe.  
year4 20 SM4-Rel4-pass-BF SM1SG-bePST with cow9
- b. Miaka ishirini i-li-yo-pit-a ni-li-ku-w-a na ng'ombe.  
year4 20 SM4-PST-Rel4-pass-BF SM1SG-PST-INF-be-BF with cow9
- (15) 'Three years ago you were a student.'
- a. Miyaka mi-tatu i-yo-pit-a kwevu (< ku-evu) mwanafuzi.  
year4 AP4-three SM4-Rel4-pass-BF SM2SG-bePST student1
- b. Miaka mi-tatu i-li-yo-pit-a u-li-ku-w-a mwanafunzi.  
year4 AP4-three SM4-PST-Rel4-pass-BF SM2SG-PST-INF-be-BF student1

Kama tunavyoona katika mifano (14) na (15), katika kauli ya njeo ya wakati uliopita kuna tofauti kubwa sana baina ya Kichaani na Kiswahili Sanifu. Katika Kichaani kitenzi -wa umbo lake

limebadilika kabisa na kuwa -evu. Lakini bado haijafafanuliwa vizuri, kwa hivyo haieleweki umbo hilo limebadilika vipi kutoka -wa na kwenda -evu. Na Kichaani kina aina mbili za kauli ya kukanusha, yaani inawezekana kutumia kiambishi cha njeo -ja- na -e- kama tunavyoona katika mifano (16) na (17). Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa kijijini, inaonekana kwamba hasa vijana wanapendelea kutumia -e- badala ya -ja-.

(16) ‘Twenty years ago I did not have a cow.’

a. Miyaka ishirini i-yo-pit-a si-ja-w-a na ng’ombe.  
 year4 20 SM9-Rel9-pass-BF NegSM1SG-IPFV-be-BF with cow9

a’. Miyaka ishirini i-yo-pit-a sekuwa (si-e-ku-w-a) na ng’ombe.  
 year4 20 SM9-Rel9-pass-BF NegSM1SG-NegPST-INF-be-BF with cow9

b. Miaka ishirini i-li-yo-pit-a si-ku-w-a na ng’ombe.  
 year4 20 SM9-PST-Rel9-pass-BF NegSM1SG-NegPST-be-BF with cow9

(17) ‘Three years ago you were not a student.’

a. Miyaka mi-tatu i-yo-pit-a hu-ja-w-a mwanafuzi.  
 year4 AP4-three SM9-Rel9-pass-BF NegSM2SG-IPFV-be-BF student1

a’. Miyaka mi-tatu i-yo-pit-a hwekuwa (hu-e-ku-w-a) mwanafuzi.  
 year4 AP4-three SM9-Rel9-pass-BF NegSM2SG-NegPST-INF-be-BF student1

b. Miaka mi-tatu i-li-yo-pit-a hu-ku-w-a mwanafunzi.  
 year4 AP4-three SM9-PST-Rel9-pass-BF NegSM2SG-NegPST-be-BF student1

Na katika kauli ya kukanusha, tukitumia kiambishi -e- katika Kichaani, kunatokea mabadiliko ya sauti hasa kwa kuwa -e- ni vokali. Tunaonyesha mabadiliko hayo katika jedwali la 2.

<Jedwali la 2: Mabadiliko ya Sauti katika Kauli ya Ukanushi wa Wakati Uliopita>

Nafsi/Ngeli	Mabadiliko ya Sauti
1SG	si-e-ku-w-a > sekuwa
2SG	hu-e-ku-w-a > hwekuwa
3SG	ha-e-ku-w-a > hekuwa
1PL	hatu-e-ku-w-a > hetwekuwa
2PL	ham-e-ku-w-a > hemwekuwa
3PL	hawa-e-ku-w-a > hewekuwa
3	hau-e-ku-w-a > hewekuwa
4	hai-e-ku-w-a > heyekuwa
5	hali-e-ku-w-a > helyekuwa
6	haya-e-ku-w-a > heyekuwa
7	haki-e-ku-w-a > hechekuwa
8	havi-e-ku-w-a > hevyekuwa
9	hai-e-ku-w-a > heyekuwa
10	hazi-e-ku-w-a > hezekuwa
11	hau-e-ku-w-a > hewekuwa

14	hau-e-ku-w-a > hewekuwa
15	haku-e-ku-w-a > hekwekuwa
16	hapa-e-ku-w-a > hepekuwa
17	haku-e-ku-w-a > hekwekuwa
18	hamu-e-ku-w-a > hemwekuwa

## 2.4 Hali Timilifu

- (18) 'She/He has become a teacher.'
- a. Ka-ma-ku-w-a            mwalimu.  
SM3SG-PFV-INF-be-BF    teacher1
- b. A-me-ku-w-a            mwalimu.  
SM3SG-PFV-INF-be-BF    teacher1
- (19) 'She/He has not become a teacher.'
- a. Ha-ja-w-a            mwalimu.  
NegSM3SG-IPFV-be-BF    teacher1
- b. Ha-ja-w-a            mwalimu.  
NegSM3SG-IPFV-be-BF    teacher1

Katika hali timilifu hakuna tofauti kubwa baina ya Kichaani na Kiswahili Sanifu, ingawa kiambishi chenyewe cha hali timilifu kinatofautiana kwa sauti.

## 2.5 Hali Timilifu Kabisa

- (20) 'You already have become a teacher.'
- a. Ku-sha-ku-w-a            mwalimu.  
SM2SG-PPFV-INF-be-BF    teacher1
- b. U-mesha-ku-w-a            mwalimu.  
SM2SG-PPFV-INF-be-BF    teacher1
- (21) 'You have not become a teacher.'
- a. Hu-ja-w-a            mwalimu.  
NegSM2SG-IPFV-be-BF    teacher1
- b. Hu-ja-w-a            mwalimu.  
NegSM2SG-IPFV-be-BF    teacher1

Katika hali timilifu kabisa hakuna tofauti kubwa sana baina ya Kichaani na Kiswahili Sanifu, kiambishi chenyewe kinatofautiana tu. Na kauli ya kukanusha ni sawasawa na ya hali timilifu.



### 3. Muundo wa Njeo Changamani / Hali Ambatani

Kama Kiswahili Sanifu hata Kichaani kinayo njeo changamani / hali ambatani. Tunaonyesha mifano kadhaa ya kauli za njeo changamani / hali ambatani.

(22) 'She/He was reading this book.'

a. Kevu (ka-evu) a-ka-som-a buku lino.  
SM3SG-bePST SM3SG-PERS-read-BF book5 DEMN5

b. A-li-ku-w-a a-ki-som-a kitabu hiki.  
SM3SG-PST-INF-be-BF SM3SG-PERS-read-BF book7 DEMN7

(23) 'Last year I used to get up early every morning.'

a. Mwaka uwopita nyevu (ni-evu) hayamuka (ni-ka-yamuk-a) usubuhi mapema kula siku.  
year3 SM3-Rel3-pass-BF SM1SG-bePST SM1SG-PERS-get up-BF morning9 early every day9

b. Mwaka u-li-o-pit-a ni-li-ku-w-a ni-na-amk-a asubuhi mapema kila siku.  
year3 SM3-PST-Rel3-pass-BF SM1SG-PST-INF-be-BF SM1SG-PRS-get up-BF morning9 early every day9

(24) 'She/He will be reading this book.'

a. Kesho ka-ta-ku-w-a kanasoma buku lino.  
tomorrow9 SM3SG-FUT-INF-be-BF SM3SG-PRS-read-BF book5 DEMN5

b. Kesho a-ta-ku-w-a a-na-som-a kitabu hiki.  
tomorrow9 SM3SG-FUT-INF-be-BF SM3SG-PRS-read-BF book7 DEMN7

(25) 'Next year I will get up early every morning.'

a. Mwaka-ni ta-ku-w-a na-yamuk-a usubuhi mapema kula siku.  
year3-LOC FUT-INF-be-BF PRS-get up-BF morning9 early every day9

b. Mwaka-ni ni-ta-ku-w-a ni-na-amk-a asubuhi mapema kila siku.  
year3-LOC SM1SG-FUT-INF-be-BF SM1SG-PRS-get up-BF morning9 early every day9

Kama inavyoonyeshwa katika mifano (22) na (23), kwa hali ya kuendelea katika wakati uliopita lazima itaje kwanza kauli yenye kitenzi -wa pamoja na kiambishi cha wakati uliopita. Na katika Kichaani tukitumia kiambishi-kiima cha nafsi ya kwanza pamoja na kiambishi cha hali ya kuendelea -ka-, silabi hizi 'nika' hubadilika kuwa 'ha'. Kwa hivyo imeandikwa 'hayamuka' badala ya 'nikayamuka' katika mfano (23).

Na kutokana na mifano (24) na (25) inafahamika kwamba kwa hali ya kuendelea katika wakati ujao pia lazima itaje kwanza kauli yenye kitenzi -wa pamoja na kiambishi cha wakati ujao.

(26) 'You have already finished to read this book.'

a. Kwevu (ku-evu) ku-sha-som-a buku lino.  
SM2SG-bePST SM2SG-PPFV-read-BF book5 DEMN5

b. U-li-ku-w-a u-mesha-som-a kitabu hiki.  
SM2SG-PST-INF-be-BF SM2SG-PPFV-read-BF book7 DEMN7

(27) 'We will have arrived Japan around this time tomorrow.'

- a. Kesho ukati kama ja uno tu-ta-ku-w-a tu-sha-fik-a Japani.  
tomorrow<sub>9</sub> time<sub>11</sub> like as DEMN<sub>11</sub> SM1PL-FUT-INF-be-BF SM1PL-PPFV-arrive-BF Japan<sub>9</sub>
- b. Kesho wakati kama huu tu-ta-ku-w-a tu-mesha-fik-a Japani.  
tomorrow<sub>9</sub> time<sub>11</sub> like DEMN<sub>11</sub> SM1PL-FUT-INF-be-BF SM1PL-PPFV-arrive-BF Japan<sub>9</sub>

Hata kwa hali timilifu katika wakati uliopita na wakati ujao pia lazima itaje kwanza kauli yenye kitenzi -wa kama tunavyoona katika mifano (26) na (27).

#### 4. Hitimisho

Katika makala hii tumeangalia miundo ya sentensi za Kichaani zenye kitenzi -wa kwa kulinganisha na sentensi za Kiswahili Sanifu. Kama tulivyotaja juu, tofauti kubwa sana iliyoko baina ya Kichaani na Kiswahili Sanifu inatokea katika sentensi za wakati uliopita / njeo iliyopita. Umbo la kitenzi chenye limebadilika kabisa kutoka -wa kwenda -evu.

Kwa sasa, mabadiliko hayo ya kitenzi -wa katika wakati uliopita bado hayajafanuliwa vizuri. Na data nyingine hasa za Kitumbatu<sup>4)</sup> zinatonyesha kuwa lahaja za Kichaani na Kitumbatu zinakaribiana zaidi kuliko Kichaani na Kiswahili Sanifu lakini hata hivyo kuna tofauti baina ya Kichaani na Kitumbatu pia kama tunavyoona katika mifano (28) na (29)<sup>5)</sup>.

(28) 'I was a student.'

- a. Nyevu (ni-evu) mwanafuzi.  
SM1SG-bePST student<sub>1</sub>
- b. Ni-li-ku-w-a mwanafunzi.  
SM1SG-PST-INF-be-BF student<sub>1</sub>
- c. Ni-vu mwanafuzi.  
SM1SG-bePST student<sub>1</sub>

(29) 'You were students.'

- a. Mwevu (mu-evu) wanafuzi.  
SM2PL-bePST students<sub>2</sub>
- b. M-li-ku-w-a wanafunzi.  
SM2PL-PST-INF-be-BF students<sub>2</sub>
- c. M-vu wanafuzi.  
SM2PL-bePST students<sub>2</sub>

---

<sup>4)</sup> Nilimhoji pia mwanamke mwingine aliyezaliwa Gomani, Kisiwa cha Tumbatu juu ya lahaja yake, lakini bado data hizo hazitoshi kabisa, nitaendelea na utafiti huu ili kuandika makala nyingine kadhaa za kulinganisha Kichaani na Kitumbatu.

<sup>5)</sup> Katika mifano hii inaonyeshwa Kichaani kwa herufi 'a', Kiswahili Sanifu kwa herufi 'b' na Kitumbatu kwa herufi 'c'.

Inasemekana kuwa ili kuhakikisha kwamba kuna tofauti kama hii baina ya Kiswahili Sanifu na lahaja zinazozungumzwa katika vijiji vingine vilivyoko karibu na kijiji cha Chaani, tunahitaji kufanya utafiti zaidi na zaidi katika eneo kubwa la Mkoa wa Kaskazini, Kisiwani Unguja, na kulinganisha na kuchambua matokeo yake.

\* Utafiti wangu huu uliendeshwa kwa msaada wa kifedha wa Wizara ya Elimu ya Japani wa mwaka wa kielimu 2011-2013. Mradi wetu wa utafiti (Namba ya mradi:(B) 23320086, Kiongozi wa mradi:Takemura Keiko, Profesa Mshiriki, Chuo Kikuu cha Osaka) unaitwa ‘Utafiti wa Lahaja za Kiswahili, Afrika ya Mashariki’.

## **Shukrani**

Kila mara nilisaidiwa na mhojiwa Marehemu Bi. ‘M’ - Mungu amlaze pahala pema peponi - aliyekuwa akikaa katika mtaa mmoja wa Chaani. Nisingekutana naye bila shaka nisingeweza kuandika makala hii, namshukuru kwa dhati yangu hasa. Mwezi wa 8 mwaka 2015 nilipata taarifa ilinihuzunisha na kunipa pigo kubwa kabisa kwamba ameaga dunia, ingawa nilitamani sana kwenda kwake lakini wapi nilikuwa nimezongwa na kazi nyingi, sikuweza kumsindikiza. Kadri ya uhai wangu, nitamkumbuka moyoni mwangu, amina!

Na tena kila mara nilisaidiwa sana na msaidizi wangu Mwl. ‘H’ pamoja na familia yake. Nilikaa na familia yake kwa muda wote nilipokuwa Chaani. Kwa msaada wao mkubwa niliweza kufanya utafiti wangu bila ya tatizo lolote, ninawashukuru mno. Halafu lazima nitaje jina lake Mwl. Zainabu kwa msaada wake mkubwa. Amenipitia na kunirekebishia makala hii kama kawaida. Ninamshukuru sana sana.

Mwishoni niongeze kutaja kwamba ikiwa kuna makosa ama kasoro ya maandiko ya makala hii, bila shaka ni wajibu wangu, si wajibu wao mhojiwa na wasaidizi wangu.

## **Vifupisho**

-	mpaka wa mofimu
1SG, 1PL	nafsi ya kwanza-umoja, nafsi ya kwanza-wingi
2SG, 2PL	nafsi ya pili-umoja, nafsi ya pili-wingi
3SG, 3PL	nafsi ya tatu-umoja, nafsi ya tatu-wingi
AP	kiambishi cha kivumishi
APPL	kiambishi-nyambulishi-utendea
BF	kiishio cha msingi
CONT	hali ya kuendelea

DEMN	kiwakilishi kionyeshi-karibu na msemaji
FUT	wakati ujao
INF	kiambishi cha -ku- ya kitenzi kisoukomo
IPFV	ukanushi wa hali timilifu
LOC	kiambishi-mahali
Neg	kiambishi-kikanushi
OM	kiambishi-yambwa
PERS	hali ya kuendelea
PFV	hali timilifu
PPFV	hali timilifu kabisa
PRS	wakati uliopo
PST	wakati uliopita
PstF	kiishio cha wakati uliopita
Rel	kiambishi-kirejeshi
SM	kiambishi-kiima

## Marejeo

- Bryan, M. A. 1959. "Swahili Group". *The Bantu Languages of Africa*. pp.126-129. Oxford University Press.
- Mkude, Daniel J. 1983. "Mtawanyiko wa Lahaja za Kiswahili". *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I - Lugha ya Kiswahili*. pp.62-83. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Nurse, D. & T. J. Hinnebusch. 1993. *Swahili and Sabaki: A Linguistic History*. University of California Press.
- Stigand, C. H. 1915. *A Grammar of Dialectic Changes in the Swahili Language*. Cambridge University Press.
- Stude, Traute. 1995. "Language Change and Language Maintenance in the Island of Tumbatu". *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. pp.83-117. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Takemura, Keiko. 2014. "On Subjunctive and Imperative Forms of Kichaani". *Swahili & African Studies* No. 25. pp.120-129. (in Japanese)
- . 2015. "Miundo ya Dhamira Matilaba na Dhamira Amri katika Kichaani". *Swahili & African Studies* No.26. pp.170-180.
- Whiteley, W. H. 1956. *Ki-mtang'ata: A Dialect of the Mrima Coast - Tanganyika*. East African Swahili Committee, Makerere College, Kampala.